

**HOTUBA YA MHESHIMIWA MAMA SALMA KIKWETE**  
**KATIKA HOSPITALI YA CHAKE CHAKE , MKOA WA KUSINI**  
**PEMBA - TAREHE 13 MEI 2010**

*Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Pemba Kusini,*

*Mhe. Mkuu wa Wilaya,*

*Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii*

*Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Bibi.  
Shawana Bukhiti*

*Mganga Mkuu wa Hospitali ya Chakechake,*

*Wafanyakazi wa Hospitali ya Chakechake,*

*Viongozi mbalimbali wa Vyama vya Siasa,*

*Wageni waalikwa,*

*Mabibi na mabwana.*

Asalaam Aleykum!

Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu,  
mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kufika salama siku  
ya leo.

Aidha nawashukuruni kwa mapokezi yenu mazuri. Nimefurahi sana kupata fursa ya kutembelea kituo cha Afya cha Chakechake leo.

Kwa kipekee nimshukuru dada yangu Mama Shadya Karume, ambaye juhudi zake katika sekta za Elimu na afya zimezaa matunda mazuri. Nami leo naungana naye katika kuziunga mkono Serikali zetu ili kuboresha afya ya mama na mtoto.

Aidha napenda niwafikishieni ujumbe kutoka kwa Mhe. Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndg. Jakaya Mrisho Kikwete, anawasalimu sana na anawatakieni kila la kheri katika shughuli zenu za kila siku.

***Mhe. Mkuu wa Mkoa, Ndugu wananchi wenzangu***

Lengo la ziara yangu hapa katika Hospitali ya Chakechake ni kutekeleza moja ya malengo ya Taasisi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA) ninayoiongoza.

Hivyo basi leo nitazungumza zaidi juu ya masuala ya afya ya uzazi, mama na mtoto, na hatimaye kutoa mchango wangu mdogo katika jitihada za kuboresha huduma ya Afya hapa Chakechake.

Sote tunatambua kuwa vifo vya wakina mama na watoto vimekuwa ni tatizo kubwa hapa Visiwani na Tanzania bara kwa ujumla. Juhudi za dhati zinatakiwa kufanywa na kila mmoja wetu ili kuhakikisha kuwa wakina mama wanajifungua salama.

***Mhe. Mkuu wa Mkoa, Maafisa wote wa afya,***

Nimefarijikia kusikia katika hotuba yenu kuwa hospitali yenu inatoa huduma muhimu za afya kama vile: **upimaji wa mama wajawazito na watoto, upimaji wa Virusi Vya Ukimwi, uzazi wa mpangilio, huduma rafiki kwa vijana wenye umri wa miaka 10-24 na ushauri nasaha kabla na baada ya kujifungua.** Huduma hizi ni za muhimu sana kwa wananchi wetu.

Napenda pia kuwapongeza kwa mafanikio mliyoyapata hasa ya kuongeza vituo vya kuzalishia kutoka vitano (5) hadi kumi na saba (17) na kuanzisha vituo viwili (2) vya huduma rafiki kwa vijana.

Hatari ya maambukizi ya UKIMWI bado ni tishio kubwa kwa vijana wetu ambao wengi wao bado hawajui namna ya kujikinga na maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI. Hili ni tatizo kubwa kwani vijana wetu ndio viongozi wetu wa taifa la kesho. Ni muhimu sana kwa sasa kuwaelekeza namna ya kutambua na kujilinda na tabia hatarishi ambazo zitaharibu maisha yao.

Pamoja na hilo afya ya uzazi kwa wasichana na wakinamama bado ni changamoto katika nchi yetu. Mikakati madhubuti bado inahitajika katika kuelimisha wananchi jinsi ya kulinda afya zao. Pia elimu itolewe kuhusu mila, desturi, mitazamo na tabia ambazo ni hatarishi katika kuongeza vifo vya akina mama na watoto wadogo pamoja na maambukizi ya gonjwa hili la UKIMWI.

Malengo mliojiwekea ya kupunguza vifo kwa wa mama wajawazito kutoka 377 kati ya vizazi hai 100,000, hadi kufikia 251 na kupunguza vifo vya watoto chini ya umri wa miaka 5 kutoka 101 kati ya watoto 1000 hadi kufikia 71 kwa mwaka huu, ni malengo mazuri sana kwani tukidhamiria hakika tutaweza, wahenga walisema **“penye nia pana njia”** .

Naomba tutambue kuwa viongozi na maafisa wa afya mnalo jukumu kubwa katika kuhakikisha wananchi wetu wanapata afya bora. Kwani afya bora ndio msingi wa maisha bora na Maendeleo kwa wananchi wetu

### ***Ndugu watumishi wa Afya, Mabibi na Mabwana***

Nimezisikia changamoto ambazo zinaikabili hospitali ya Chakechake, katika kutoa huduma za afya ya mama na mtoto. Naamini kupitia mkutano huu wadau wengi zaidi wamezisikia pia na kila mmoja atatimiza wajibu wake kutokana na nadasi aliyonayo.

Kwa upande wa WAMA leo tumekuja kuwaunga mkono kwa kuwaletea vifaa vifuatavyo:

- Kivunge cha kuwekea vifaa vya kujifungulia (Delivery Kit) kimoja (01)  
Kivunge hiki ni cha kisasa, kina vifaa vya operesheni ndogo (caesarean kit) na huwa vinadawa ya kusafishia (self sterilization)
- Kifaa cha kuvutia uchafu kwa watoto wanaozaliwa (Suction pump) kimoja (01)
- Toroli la kubebea vifaa vya huduma wodini (Dressing Trolley)
- Mzani wa watoto (Infant Scale)
- Vitanda vya hospitali (2)
- Magodoro (2)
- Mashuka (4)

Ni matumaini yangu kuwa, vifaa hivi vitasaidia kwa kiwango fulani kuboresha huduma ya afya ya uzazi. Kwani Wahenga walisema **“Ndondo si Chururu”**

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA!**